

**HOTUBA YA MHE. SAIDI M. SADIKI, MKUU WA MKOA
WA KILIMANJARO KATIKA SIKU YA UZINDUZI WA
UTAYARISHAJI MPANGO KABAMBE (MASTER PLAN) WA
MJI MOSHI KATIKA UKUMBI WA MKUU WA MKOA
TAREHE 10 APRILI, 2017**

- Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi;
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Moshi na Hai;
- Waheshimiwa Wabunge;
- Waheshimiwa Madiwani;
- Katibu Tawala wa Mkoa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Makatibu Tawala wa Wilaya;
- Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri;
- Wataalamu mbalimbali;
- Wageni Waalikwa;
- Wandishi wa Habari;
- Mabibi na Mabwana:

Nashukuru kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika kikao hiki cha uzinduzi wa utayarishaji wa Mpango Kabambe wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

Ndugu washiriki, Mpango Kabambe ni matokeo ya uhitaji wa kuwa na chombo kitakachoongoza ukuaji wa miji. Ukuaji wa miji ni muhimu sana ukazingatia hali ya kimazingira ambayo ni wezeshi na ya kupendeza. Mpango Kabambe huzuia miji inayokuwa kwa kasi kuwa na ongezeko la makazi holela, ongezeko la idadi ya watu wasio na huduma za msingi kama afya, maji na barabara na kuwafanya wakazi wake waweze kuishi katika hali bora zaidi.

Ndugu washiriki, Tanzania ina historia katika kuandaa mpango kama huu katika miji mbalimbali kwa nyakati tofauti tofauti. Mpango kama huu kwa mara ya kwanza nchini Tanzania uliandaliwa na Sir Alexander Gibbs katika mji wa Dar es salaam mwaka 1948 ambayo ilikuwa kabla ya uhuru. Hii ilifuatiwa na miji mingine kama Mtwara mwaka 1968. Mikoja mingine iliyofuatia katika kuandaa mpango kama huu ilikuwa ni Mwanza, Iringa, Mbeya, Morogoro, Tanga, Arusha na Mji wa Moshi ambao uliandaa mpango wake kabambe kwa mara ya kwanza mwaka 1974. Wakati huo mji wa Moshi ulikuwa na eneo la kilomita za mraba 23, baadae ikaanda Mpango Kabambe wa pili mwaka 1995-2015 ikiwa na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 58.

Kwa sasa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi iko kwenye maandalizi ya mpango mpya wa mwaka 2017-2037 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 142, hii ni kwa mujibu wa Gazeti la Serikali namba 219 la Tarehe 15 Julai 2016 ambapo imejumuisha kilomita za mraba 68 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na kilomita za mraba 16 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Masuala yote ya upanuzi wa Manispaa yamewezekana baada ya kuzijulisha ngazi zote za kiutawala kuazia chini hadi Taifa.

Ndugu washiriki; Uandaaji wa Mipango Kabambe unazingatia sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mipangomji ya mwaka 2007, Sera ya Makazi ya mwaka 2000 nk. Miongozo hii inatoa maelekezo ya uandaaji wa mpango kabambe ambao utaongoza ukuaji wa miji na usimamizi wa maendeleo ya miji ili kuwa na miji endelevu na inayokalika kwa watu wote.

Ndugu washiriki, kukosekana kwa Mipango Kabambe kumeifanya miji kukua kiholela kwa kuwa na makazi yasiyopangwa, na yasio na fursa za kimaendeleo ya uwekezaji na uchumi, kutumia rasilimali kusiko endelevu. Kukosekana kwa Mipango Kabambe kunafanya miji mingi kuwa tegemezi badala ya

kuzalisha. Madhumuni ya mpango huu ni kuratibu maendeleo endelevu ya Manispaa ya Moshi ili Manispaa yetu iweze kuimarika kiuchumi, kiafya, kiusalama, kuwa na hali nzuri na ya kupendezesha, ustawi pamoja na ufanisi katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi.

Ndugu washiriki; Kukamilika kwa utayarishaji wa Mpango Kabambe huu kutatoa uelekeo wa kuboresha mazingira wezeshi kwa kutumia ardhi katika utoaji wa huduma mbalimbali ambazo ni muhimu katika ustawi wa jamii kama vile kutenga maeneo ya miundombinu, kilimo, hifadhi, viwanda makazi na sehemu za biashara.

Ndugu washiriki; Natambua uandaaji wa mpango huu utachukua mwaka mmoja ukiwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ya Mji wa Moshi na Wilaya jirani za Hai na Moshi. Vilevile, Mji wa Moshi ndio Makao Makuu ya Mkoa, pia ni Makao Makuu ya Kanda ya Kaskazini ambapo taasisi mbalimbali zimeanzisha Ofisi na unatarajia kuwa Jiji kabla ya mwaka 2020. Hivyo, kuandaliwa kwa Mpango Kabambe kutachochea ukuaji kiuchumi kwa wilaya zingine na Mkoa kwa ujumla na pia kuharakisha Manispaa kupandishwa hadhi kuwa Jiji.

Napenda kuwasihi viongozi na wananchi wote kutoa ushirikiano kwa wataalamu washauri waliopewa kazi ya kuandaa Mpango Kabambe wa Mji wa Moshi ambao utajumuisha baadhi ya maeneo ya Wilaya za Moshi na Hai. Ni matuamini yangu kuwa nyote mliopo hapa mtakuwa mabalozi wa mpango huu. Sitarajii kuwa na malumbano ya kisiasa bali tuangalie maslahi ya wananchi watakayopata kutokana na mpango huu. Tuache ubinafsi.

Baada ya kusema haya machache, natamka kwamba; **uzinduzi wa uandaaji wa Mpango Kabambe wa Mji wa Moshi umezinduliwa rasmi leo tarehe 10/04/2017.**

Asanteni Sana kwa Kunisikiliza.